

**HOTUBA YA MHE. CHARLES MAKONGORO NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA KUMUAPISHA MHE. MKUU WA WILAYA YA SUMBAWANGA TAREHE 06 OKTOBA, 2023**

- *Mwenyekiti wa CCM Mkoa,*
- *Kaimu Katibu Tawala Mkoa,*
- *Katibu wa CCM Mkoa,*
- *Kamati ya Usalama MKoa,*
- *Wahe. Wakuu wa Wilaya,*
- *Wakuu wa Seksheni na Vitengo,*
- *Makatibu Tawala Wilaya,*
- *Mstahiki Meya wa Manispaa ya Sumbawanga*
- *Wenyeviti wa Halmashauri,*
- *Wakuu wa Seksheni na Vitengo wa Sekretarieti ya Mkoa,*
- *Makatibu Tawala wa Wilaya (Sumbawanga, Kalambo na Nkasi),*
- *Wahe. Wabunge,*
- *Mstahiki Meya wa Manispaa ya Sumbawanga,*
- *Wahe. Wenyeviti wa Halmashauri (Sumbawanga, Kalambo na Nkasi),*
- *Wakurugenzi wa Halmashauri,*
- *Waandishi wa Habari,*
- *Wageni waalikwa,*

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....***

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kuwa hapa leo tukiwa na afya njema. Kipekee nimpongeze Mhe. Sixtus Raphael Mapunda Mkuu wa

Wilaya ya Temeke kwa utumishi uliotukuka katika Wilaya ya Sumbawanga. Ulikuwa ni mhimili mkubwa wa Wilaya ya Sumbawanga ukizingatia kuwa Wilaya ya Sumbawanga ni Makao Makuu ya Mkoa wa Rukwa. nilipenda Programu yako ya Kliniki ya Ardhi ambayo kwa kiasi kikuwa ilipunguza migogoro ya ardhi.

***Ndugu Wajumbe***, Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga uliyeapa leo una kazi kubwa ya kuhakikisha kuwa miradi kwenye Wilaya yako inakamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa. Aidha, suala la usafi kwenye Manispaa yetu ya Sumbawanga bado ni changamoto. Simamia usafi kwenye Wilaya yako.

***Mwisho***, lakini si kwa umuhimu, simamia ulinzi na usalama kwenye eneo lako, ukusanyaji wa Mapato, utatuzi wa kero za Wananchi na huduma bora kwa wananchi. Aidha, simamia ufanyikaji wa Vikao vya Kisheria ngazi ya Mitaa, Vijiji, Kata na Halmashauri ili vifanyike kwa Mujibu wa Sheria.

Mungu Ibariki Tanzania

Mungu bariki Mkoa wa Rukwa

Asanteni kwa kunisikiliza

Charles Makongoro Nyerere

**MKUU WA MKOA WA RUKWA**